THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

015/1

# ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 1

*(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)*

Muda: Saa 2 — Ijumaa Novemba 05, 2004 Mchana

---

*Maelekezo*

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Mashine za hesabu za elektroniki **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

*Karatasi hii ina kurasa 8 zenye maandishi.*

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

**Bismillahir - Rahminir - Rahiim.**

## SEHEMU A: SUNNAH NA HADITHI (Alama 10)

1. Kwa maswali (i) – (x) chagua jibu lililo sahihi kwa kila swali kisha andika herufi ya jibu hilo kando ya namba ya swali husika katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Ipi ni maana ya Sunnah ya Mtume (s.a.w.) kiutendaji?

A "Na hazungumzi (Muhammad anayozungumza) kwa matamanio yake. Isipokuwa (anayozungumza) ni wahyi uliofunuliwa kwake. (53:3-4)

B Sunnah ya Mtume (s.a.w.) ni yale matendo ya msingi aliyoyafanya, aliyoyaagiza, aliyoelekeza na yaliyofanywa mbele yake bila kuyakemea au kuyakataza

C Taarifa juu ya matendo ya Mtume (s.a.w.) ambayo ni sehemu ya utume wake

D Kufuata matendo ya maswahaba wa Mtume (s.a.w.) na kuacha yale yaliyokemewa na maimamu waliofuatia

E Kufanya yale Mtume (s.a.w.) aliyoyaamrisha na kuyaacha yale aliyoyakataza.

(ii) Sunnah ya Mtume (s.a.w.) ni muhimu sana katika kuutekeleza uislamu kwa sababu ipi?

A "Na anachokupeni Mtume basi pokeeni na anachokukatazeni jiepusheni nacho." (59:7)

B "Na hazungumzi (Muhammad anayozungumza kwa matamanio yake. Isipokuwa anayozungumza ni) wahyi uliofunuliwa kwake." (53:3-4)

C "Hii ni kawaida ya Allah (ya kuwaadhibu wakorofi) iliyokuwa kwa waliopita zamani kutopata mabadiliko katika kawaida ya Allah." (33:62)

D "Je, hawayajui ya kwamba anayeshindana na Mwenyezi Mungu na Mtume wake, basi yeye atapata moto wa Jehanamu kukaa humo daima? " (9:63)

E Ndiyo njia pekee ya kuwafundishia wafuasi wa Mtume (s.a.w.) ili waongoke.

(iii) Katika kipindi cha uhai wa Mtume (s.a.w.) ipi **si** sababu ya uandishi duni wa Hadithi?

A Mtume mwenyewe alikuweko

B Maswahaba walishughulika zaidi na uandishi wa Qur-an iliyokuwa inamshukia Mtume (s.a.w.)

C Maswahaba walizoea kutoandika kwa kuwa mwanzo walikatazwa na Mtume (s.a.w.)

D Maswahaba walikuwa hawajui kusoma wala kuandika

E Maswahaba wengi walikuwa na uwezo mkubwa wa kuzihifadhi hadithi vifuani mwao.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(iv) Ni tukio lipi lililotokea katika kipindi cha Maswahaba na kufanya uandishi wa Hadithi za Mtume (s.a.w.) kuwa muhimu?

A Kupanuka kwa dola ya Kiislamu
B Kutwawafu kwa Mtume (s.a.w.)
C Kuzuka kwa vita
D Kuzuka kwa hadithi nyingi za uongo
E Kutoweka kwa Maswahaba wa Mtume (s.a.w.).

(v) Kitabu cha Hadithi kilichoandikwa na Hazrat Ali kilijulikana kwa jina lipi?

A Al – Waqidi
B Shuwabul – Iman
C Al – qatadaya
D Al-Muwatta
E Nabawiy.

(vi) Mwandishi mashuhuri wa Hadithi aliyeishi katika kipindi cha Tabiin alijulikana kwa jina lipi?

A Anas bin Malik
B Imam Malik bin Anas
C Abu Hanifa al-Muman bin Thabit
D Said bin Abi Ubaidah
E Sayyidina Omar bin Al-Khataab.

(vii) Matin ya Hadithi ya Mtume (s.a.w.) maana yake ni ipi?

A Kauli au matendo ya Mtume (s.a.w.)
B Mapokezi ya hadithi zaidi ya moja
C Kigezo cha usahihi wa Isnad
D Taarifa juu ya Sunnah
E Ufafanuzi wa Qur-an tukufu.

(viii) Ipi ni tofauti baina ya Isnad na Riwaya?

A Isnad ni msururu wa wapokezi wa Hadithi wakati Riwaya ni maelezo ya Matin
B Riwaya ni Isnad na Matin; Isnad ni historia ya wapokezi
C Isnad ina Matin na Riwaya ni msururu wa wapokezi tu
D Riwaya ni Matin ambapo Isnad ni sifa ya mpokezi wa Hadithi
E Isnad ni msururu wa wapokezi wakati Riwaya ni Matin moja pamoja na Isnad.

(ix) Hadithi "Hasan" ni hadithi ya aina ipi?

A Hadithi yenye kukubalika pasi na shaka
B Hadithi iliyopokewa na watu wengi
C Hadithi inayofanana na Hadithi sahihi isipokuwa wasimulizi wake wana udhaifu
D Ni usemi alioutoa Mtume (s.a.w.) kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa njia ya ilhamu
E Taarifa juu ya matendo ya Mtume (s.a.w.).

(x) Hadithi iliyo katika daraja ya juu kabisa kwa usahihi ni ile iliyopokewa na

A Sahihi Bukhari na Muslim
B Sahihi Muslim na Ibn Majah
C Sahihi Muslim na At-Tirmidh
D Sahihi Bukhari na Nnawawi
E Sahihi Majah na Bukhari.

Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU B: QUR-AN (Alama 15)

2. Chagua kutoka **ORODHA B** kifungu kinachowiana na kifungu kutoka **ORODHA A**. Kwa mfano, kifungu (i) cha orodha A kinawiana na kifungu (a) cha orodha B. Jibu ni (i) = (a).

**ORODHA A**

(i) "Hayakuwa haya (anayosema) ila ni wahyi (ufunuo) uliofunuliwa (kwake). Amemfundisha (Malaika) mwenye nguvu sana". (53:4-5).

(ii) "Basi alipoufikia aliitwa kutoka upande wa kuliani wa bonde hilo katika kiwanja kilichobarikiwa kutoka mtini, Ewe Musa! Bila shaka Mimi ndiye Mwenyezi Mungu, Mola wa Walimwengu." (28:30).

(iii) "Na hakuwa mwenye kusoma kitabu chochote kabla ya hiki, wala hukukiandika kwa mkono wako wa kuume, ingekuwa hivyo, wangefanya shaka wale wanaotaka kubadilisha (haki)." (29:48).

(iv) "Ni mwezi Ramadhani ambao imeteremshwa Qur-an ili iwe uongofu kwa watu na ubainifu wa hoja zilizo wazi kwa uongozi na upambanuzi (wa haki na batili)" (2:185).

(v) "Au ndio wanasema kuwa hii (Qur-an) ameitunga (yeye mwenyewe Muhammad)? Basi wao hawaamini lolote." (52:33).

(vi) "Na kama ukiwatii wengi katika (hawa) waliomo ulimwenguni watakupoteza na njia ya Mwenyezi Mungu. Hawafuati ila dhana (tu) na hawakuwa ila wenye kuzua tu." (6:116).

(vii) Mara tu alipoumbwa Nabii Adam (a.s.) alipewa elimu na Mola wake. Rejea Qur-an (6:31).

(viii) "Bali hii Qur-an tukufu (iliyotolewa) katika huo ubao uliohifadhiwa." (85:21-22).

(ix) Lengo la elimu kwa Muislamu ni kumfikisha katika ucha-Mungu.

(x) "Haitakufikia batili mbele yake wala nyuma yake kimeteremshwa na mwenye hikima ahimidiwaye." (41:42).

(xi) "Usiutikise ulimi wako kwa (kufanyia haraka) wahyi. Kwa hakika ni juu yetu kuukusanya na kuusomesha" (75:16-17).

(xii) "Hakika sisi ndio tulioteremsha mawaidha haya na hakika sisi ndio tutakaoyahifadhi." (15:9).

(xiii) "Na bila shaka tunajua kwamba wanasema yuko mtu anayemfundisha (lakini) lugha ya yule wanayemuelekeza ni ya kigeni; na hii lugha inayotumika katika Qur-an ni lugha ya Kiarabu bulbul." (16:103).

(xiv) "Hawazingatii nini hii Qur-an? Na kama ingelitoka kwa asiyekuwa Allah bila shaka wangelikuta ndani yake hitilafu nyingi." (4:82).

(xv) "Na ikiwa mna mashaka kwa haya tuliyomteremshia Mtume wetu, basi leteni sura moja iliyofanywa na (mtu) aliye mfano wake..." (2:23).

(xvi) "Lakini (makafiri) wakisema (hayo anayosimulia) ni ndoto zilizovurugika. Bali ameyabuni (mwenyewe). Bali huyu ni mtunga mashairi tu..." (21:5).

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

**ORODHA B**

A Qur-an (96:1-5).

B "Hakika sisi tumeteremsha Qur-an katika usiku mtukufu wenye cheo." (97:1).

C Ushahidi kuwa Qur-an ni kitabu cha Allah (S.W.).

D "Basi muamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake aliye Nabii Ummy." (7:158)

E Madai ya makafiri dhidi ya Qur-an hayana msingi wowote.

F Njia za mawasiliano kati ya Mwenyezi Mungu na wanadamu.

G Qur-an imebakia katika asili yake tangu iliposhushwa hadi leo.

H Wala msiseme kwa sababu ya uwongo usemao ndimi zenu. Hii ni halali na hii ni haramu. Msije mkamzulia uongo Mwenyezi Mungu. Hakika wale wamzuliao uwongo Mwenyezi Mungu hawatafaulu.

## SEHEMU C: TAUHIID (Alama 15)

3. Panga vipengele vya (a), (b) na (c) katika mtiririko wenye kuleta mantiki.

(a) Mtazamo wa Uislamu juu ya maana ya dini unaelezeka kama ifuatavyo:

(i) Uislamu ndiyo dini pekee inayomletea mwanadamu faraja na furaha kwa sababu imetumwa na Allah (S.W.) aliye mjuzi na mwenye hikima.

(ii) Hivyo, tafsiri ya makafiri kuwa dini ni imani juu ya Mungu Muumba si tafsiri sahihi.

(iii) Dini ni mfumo wa maisha anaoufuata mwanadamu katika kuendesha maisha yake ya kila siku ya kibinafsi na ya kijamii.

(iv) Dini ziko nyingi lakini Uislamu ndiyo dini pekee anayoiridhia Allah (S.W.) kama Qur-an inavyosisitiza: "Bila shaka dini mbele ya Allah ni Uislamu." (3:19).

(v) Dini isiyokuwa ya Allah (S.W.) humuelekeza mwanadamu kwenye maisha ya upotevu yenye dhiki na dhuluma.

(b) Kuamini Akhera ni kuwa na yakini moyoni juu ya

(i) Kuishi ama motoni au peponi

(ii) Kuhesabiwa na kuhukumiwa

(iii) Kufikwa na mauti

(iv) Kuishi kiroho kaburini (Barzakh)

(v) Kufufuliwa na kukusanywa kwenye uwanja wa hesabu.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(c) Kwa mujibu wa Qur-an na Hadithi sahihi za Mtume (s.a.w.) imani ya Kiislamu imejengwa juu ya nguzo zifuatzo

(i) Kuamini vitabu vya Mwenyezi Mungu na kufahamu kuwa lengo la vitabu hivyo ni kumwongoza mwanadamu katika njia iliyonyooka.

(ii) Kuamini malaika wa Mwenyezi Mungu ni kutambua kuwa wao ni viumbe wake aliowaumba kwa lengo la kumtumikia yeye tu.

(iii) Kuamini Mitume wa Allah (S.W.) kwa kufahamu ujumbe wao na kuigiza mienendo yao katika maisha yetu ya kila siku.

(iv) Kumwanini Mwenyezi Mungu (S.W.) kwa kuyakinisha kuwapo kwake kwa kutafakari ishara zake mbalimbali na kuzijua sifa za Mwenyezi Mungu.

(v) Kuamini siku ya mwisho na kuamini Qadar ya Allah (S.W.).

## SEHEMU D: FIQH (Alama 30)

4. Jibu kwa kifupi kwa kujaza nafasi zilizo wazi katika maswali (i) – (xv). Andika neno au maneno yanayokosekana tu, katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Nyenzo muhimu alizopewa baba yetu Adam (a.s.) kabla ya kuletwa ardhini kuwa ____________ ni ____________ ya mazingira ya baadaye akapelekewa mwongozo na Mola wake.

(ii) Nguzo ya kwanza ya imani na ile ya Uislamu zote zinasisitiza juu ya __________ Mwenyezi Mungu na ____________ na chochote.

(iii) Aliyetoa shahada ya kweli ni yule anayeendesha maisha yake yote kwa kufuata _________ na ___________ katika kila kipengele cha maisha yake.

(iv) "Hakika wamefuzu waumini na - - - Na ambao swala zao huzihifadhi" (23:1-2, 9). Kuhifadhi swala ni kutekeleza _________ na ____________ za swala.

(v) Muislamu anapopatwa na hadithi kubwa au ya kati na kati ataoga kwa kuzingatia nguzo (a) ___________ na nguzo (b) ______________

(vi) Nguzo za swala ya maiti ni (a) Nia (b) ________ (c) ________ (d) Takbira nne (e) Kutoa salamu ya mwisho.

(vii) Muislamu atalazimika kutoa Zakat iwapo ana mali iliyofikia Nisaab. (a) Nisaab ya Ng'ombe ni ____________ (b) Nisaab ya Shahamu ni _____________

(viii) Utoaji wa Zakat na Sadaqat utafikia lengo iwapo mtoaji atajiepusha na (a) Chumo la haramu, (b) ______________________, (c) ________________ na (d) kutoa vilivyo vibaya.

(ix) Kwa nini Waislamu tumefaradhishwa kufunga katika mwezi wa Ramadhani?

(x) Mambo yanayoharibu funga (swaumu) ya mtu ni (a) ______________ (b) ___________

(xi) Moja ya masharti ya Tawat (kutufu) ni ________________

(xii) Siku ya kuchinja (mwezi 10 Dhul-Hija) Muislamu anayehiji Hija ya Al-Qiran analazimika kufanya yafuatayo: (a) Kutupa mawe Jamaratul Aqaba (b) _________________ (c) ___________ (d) Kutufu tawaful ifadha.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(xiii) Ndoa katika Uislamu ni suala muhimu sana ili kuiepusha jamii na ____________ na kujenga ____________, huruma na ushirikiano katika familia.

(xiv) Biashara katika Uislamu inaweza kuwa haramu kwa kutoifuata misingi iliyowekwa na ____________ au ikiwa ni mauzo ya ____________ zilizoharamishwa moja kwa moja.

(xv) Usia unaoruhusiwa katika Uislamu ni ____________ ya mali yote ya marehemu baada ya kutoa gharama za mazishi, Zaqat na ____________

## SEHEMU E: TAREKH (Alama 30)

5. Chagua neno au maneno (1) – (32) ili ukamilishe kauli (i) – (xv) kwa usahihi. Kwa mfano, Maneno (1) na (2) yanaifanya kauli (i) kuwa sahihi; jawabu ni (i) = (1,2).

**Maneno/Vifungu vya Maneno:**

1. Nyani
2. Adam (a.s.)
3. Jahiliyah
4. Mlezi Mkuu ni Allah (S.W)
5. Kudharauliwa
6. Uzushi
7. Imani
8. Abu Jahal
9. Qaynuka
10. Usaliti
11. Haki
12. Makka
13. Kujitoa muhanga
14. Utii
15. Viongozi
16. Badr
17. Subra
18. Kudhihakiwa
19. Utovu wa maadili na ushirikina
20. Kujielimisha
21. Maqureysh
22. Daru-al – Nadwa
23. Ka' aba
24. Kutaka kumuua Mtume
25. Nadhir
26. E A M W S
27. Kumtukuza Mwenyezi Mungu
28. Kibri
29. Afrika ya Mashariki
30. Iblisi
31. Mkataba
32. Uongozi.

**MASWALI**

(a) Kwa mujibu wa Qur-an, asili ya mwanadamu si __________ bali ametokana na kizazi cha ____________

(ii) ____________ amelaaniwa na Mwenyezi Mungu kwa kuwa na _________ cha kutotii amri ya Muumba wake.

(iii) ____________ na ____________ ni miongoni mwa mateso ya kisaikolojia aliyoyapata Nabii Nuhu (a.s.) kutoka kwa wapinzani wa ujumbe wa Mwenyezi Mungu.

(iv) Kipindi chote cha Karne ya sita kabla ya Mtume Muhammad (s.a.w.) kiliitwa __________ kwa sababu ya ____________ waliokuwa nao wakazi wa Bara Arab na kwingineko ulimwenguni.

(v) Kuwachagua __________ wenye historia nzuri kuanzia utotoni na kuwa ______ ni miongoni mwa mafunzo tunayoyapata kutokana na malezi ya Mtume Muhammad (s.a.w.) kabla ya kupewa Utume.

(vi) ____________ na ____________ ni kanuni za msingi za awali alizopewa Mtume (s.a.w.) na hivyo, Waislamu katika kuusimamisha Uislamu katika jamii hawana budi kuzifuata.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(vii) ____________ ni mojawapo ya njama za Makureysh kuupiga vita Uislamu wakati wa Mtume akiwa ______________.

(viii) Mateso waliyofanyiwa Waislamu katika kipindi cha Mtume hayakuwatetereshа bali yalianzisha ________________ na ________________

(ix) _______________ na _____________ ni mazingatio muhimu sana kwa Waislamu wa leo yanayotokana na Hijra ya Mtume kwenda Madinah.

(x) Mkutano ulioitishwa na ___________ kujadili kumuua Mtume (s.a.w.) ulifanyika katika _______________

(xi) Katika uendeshaji wa serikali ya Kiislamu Madinah, Mtume aliwekeana ____________ wa amani na wasiokuwa Waislamu uliolinda ______________ zao.

(xii) _______________ na ______________ ni makabila ya Kiyahudi yaliyovunja maelewano na Mtume (s.a.w.) na kutangaza uadui na Waislamu.

(xiii) Vita vya _____________ ni matokeo ya chokochoko za muda mrefu za ___________ dhidi ya dola changa ya Kiislamu Madinah.

(xiv) ____________ na ____________ ni baadhi tu ya vituko vya wanafiki dhidi ya Mtume na Waislamu Madinah.

(xv) Moja ya mafanikio makubwa ya mkataba wa Hadaibiyya ni kuifanya ____________ kuwa chini ya ____________ wa Waislamu.

(xvi) ___________ ni taasisi iliyokuwa na lengo la kuutangaza Uislamu ________ toka ilipoanzishwa mwaka 1933.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org